## Video ya 1: Ukweli wa musingi ju ya Finland

**Hii ni video kwa ajili ya wakimbizi wenye wameenda kuishi huko Finland**

**Finland ni inchi ya hali gani?**

- Finland ni inchi ndogo sana , ambayo inapatikana ku Nord ao kaskazini duniani  inapatikana kati ya Suèd na Russie.
- Capital na ville kubwa ni Helsinki , lakini kuna mitaa nyingi midogo inchini Finland ambao kunaishi ma elfu ndogo za watu.
- Population mzima ya Finland ni kama watu millioni tano na nusu
- Finland ni inchi ya amani ambayo inaheshimu haki za binadamu

**Finland inakaa namuna gani?**

- Upande kubwa ya Finland imezungukwa na musitu na lacs, lakini pia kuna villes na municipalités chache katika sehemu mbalimbali ya inchi.
- Majengo ni muzuri na iko très développé.
- Inchini Finland kuna maeneo chache yenye iko na poplulation kubwa. Kwa hivyo nafasi mingi iko bure bila watu na maisha en général ni ya amani na ya mupangilio muzuri.
- Villes na mashambani ni safi na imetunzwa muzuri. Lazima watu watupe takataka yao yote kwenye mapipa ya takataka.

**Watu wa Finland wanaongea lugha gani?**

- Langues officiel ya Finland ni Finnois na Suédois.
- Kuna certaines municipalités ambapo watu wanaoongea Suédois ni wengi kuliko watu wengine.
- Watu wengi wa Finland wanaongea Kiingereza, lakini ili kujua Finnois na Suédois lazima wajifunze huko shuleni na kazini.
- Kwa sababu watu kutoka inchi ya mbali wanahamia huko, watu wengi sasa wanaongea lugha ya Russe, Estonien, Arabe  na malugha ingine ya kigeni.

**Climat ya Finland iko namuna gani?**

- Kuna saisons ine tofauti: l'hiver, printemps, l'été na l'automne.
- L'hiver iko na baridi na neje, lakini ndani ya nyumba na bâtiments publics, iko joto kila wakati mwaka muzima.
- Hata wakati wa l'hiver, watoto wanenda shule na watu wazima wanenda kazini.
- Wakati wa printemps, neje inayeyuka na musimu wa mumea kumea unaanza.
- L'été ni kipindi ya joto, na kila kitu iko rangi ya verte.
- Watoto wa shule na watu wa kwenda kazini wanapewa vacance murefu wakati wa l'été.
- Wakati wa l'automne, climat inaanza kuwa baridi sana na mumea mingi inaanza kuangusha les feuilles.

**District du gouvernement iko namuna gani huko Finland?**

- Inchi imegawanywa katika régions, na kila région imegawanywa katika municipalités.
- Municipalité inamaanisha sehemu ya gouvernance ile inapanga huduma ya watu wake. Inaweza kuwa ville ndogo au ville kubwa.
- Kila région inchini Finland iko na histoire tofauti na traditions yao wenyewe.

- Immediatement ukifika Finland, utaenda kwenye municipalité na kwa nyumba yako mwenyewe ya kukodisha.

**Les événements historiques muhimu sana ni gani?**

- Kama ilivyo kwa mainchi mingi, hapo zamani Finland ilikuwa attaqué na ikapigana vita.
- Finland ilikuwa sehemu ya Royaume de Suède kwa mwaka 600 na baadae sehemu ya Empire Russe kwa mwaka 100, lakini Finland ilikuwa inafanya maamuzi yake peke yake.
- Finland ilipata uhuru mwaka 1917. Muda muchache baadae kulikuwa na guerre civile mwaka 1918.
- Watu wa Finland waliungana wakati walipigana na Union Soviétique katika Vita ya Pili ya Dunia.
- Zamani watu wengi wa Finland walikuwa na umasikini, njaa na misère.
- Baada ya guerre civile, walijenga tena Finland na sasa imekuwa inchi muzuri.
- Finland haijapigana vita na inchi ingine yoyote tangu 1945.
- Finland iliungana na Union Européene mwaka 1995.

**Système politique ya Finland iko namuna gani?**

- Finland ni République ya Kidemokrasia.
- Rais ndiyo mukuu wa serikali inchini Finland.
- Mwanamuke na mwanaume wamewai kuchaguliwa kuwa mukuu wa inchi ya Finland.
- Parlement iko na wabunge 200 na wanawakilisha partis na mutazamo mingi tofauti ya kisiasa.
- Watu wote wa Finland wa zaidi ya miaka 18, wako na haki ya kupiga kura.
- Watu wa inchi ingine wako na haki ya kupiga kura baada ya kuishi inchini Finland kwa miaka mbili.

**Sheria ya Finland inalinda haki ya watu namuna gani?**

- La constitution ya Finland inasema kila mutu anayeishi Finland ako na haki kama ya watu wengine na wote sont égaux bila kujali inchi yake, umri, sexe, afya au sababu ingine.
- Wakimbizi ni partie de la communauté na wako na haki na kazi sawa kama watu wengine wa Finland.
- Wanawake na wanaume sont égaux inchini Finland. Kila mutu ako na haki ya kutoa maoni yake na uhuru wa kuvaa nguo vile anataka.
- Hakuna mutu anaweza kuhukumiwa kifo au kuteswa.
- Watoto, bibi na bwana au mutu ingine hawezi kunyanyaswa; hawezi kuchapwa, kupigwa makofi, kuvurutwa nywele, au kunyanyaswa kwa njia ingine.
- Unyanyasaji wa kisaikolojia est interdit.
- Circoncision féminine na kunyanyasa watu sont interdit.
- Inchini Finland, maafisa, pamoja na polisi, ni watu muhimu sana na wanaheshimika kwa sababu kazi yao ni kusaidia na kulinda wanainchi. Kutokana na recherche, 95% ya watu wa Finland wanafikiria polisi ni watu wa kuaminika.
- Hakuna sababu ya kuogopa afisa yoyote.
- Finland ni moja ya inchi yenye kiwango ya chini ya corruption duniani.

**Religion principale  inchini Finland ni gani?**

- Religion principale ya Finland ni Ukristo na watu wengi wa Finland wanaenda kanisa ya Injili ya Eglise Luthérienne.
- Religion inaonekana kama kitu ya mutu binafsi na haina jukumu kubwa sana katika maisha ya watu.
- Idadi ya musulmans inaongezeka inchini Finland na kuna mosquées mingi katika municipalités kubwa kubwa.
- Kuna uhuru ya religion inchini Finland, yaani kila mutu ako na uhuru wa kuwa katika communauté ya religion na kufanya mambo ya religion, na pia wako na uhuru ya kukataa religion.

**Communauté ya watu wa Finland iko namuna gani?**

- Tangu kupata indépendance, Finland imepitia mabadiliko makubwa.
- Finland ilianzia économie ya kilimo ya chini na kubadilika na kukuwa société ya technologie, mahali technologie, habari na huduma inafanya kazi muhimu katika kutengeneza utajiri ya inchi.
- Inchi na municipalités inahakikisha kuna huduma ya kutosha ya kijamii na afya kwa wanainchi wote. Huduma hii inatoka kwa les impôts ya watu wa Finland.
- Wanainchi wote, pamoja na wakimbizi wanalipa les impôts ili kudumisha système ya prospérité ya Finland pamoja na elimu, afya, huduma ya infrastructure ya société publique.
- Kwa hivyo, ni muhimu kujifunza lugha ya Finnois na Suédois na kujitayarisha kusoma na kufanya kazi.
- Wanawake na wanaume sont égaux huko Finland na wote wanatarajiwa kufanya kazi.
- Kuna wanawake wengi wanafanya kazi kubwa katika siasa, kazini na maeneo ingine ya jamii.
- Tangu miaka ya 1990 Finland imeendelea kukuwa na traditions mingi zaidi na iko na watu kutoka mainchi na makabila mingi tofauti. Ingawa unaweza kukabiliana na xénophobie au ubaguzi wa rangi kama mahali pengine popote, watu wengi wa Finland ni marafiki.

**Familia za Finland iko namuna gani?**

- Familia ya musingi inchini Finland kwa kawaida ni wazazi na watoto.
- Ingawa watu wa Finland kwa kawaida wanaona wazazi au grand-parents kama familia ya karibu, mara mingi hawaishi pamoja.
- Huko Finland, homosexuels, lesbiennes na transgenres wako na haki ya kukuwa na relations.
- Ni kitu ya kawaida na inakubalika kwa watoto wa miaka 18 kuhama na kuishi mbali na wazazi.
- Watoto sio lazima wasaidie wazazi na pesa.

**Ni nini muhimu kwa watu wa Finland?**

- Watu wa Finland wanaheshimu kuweka siri, kuwa muaminifu na ponctualité.
- Kwa jumla, watu wa Finland wanapenda afya njema, familia, kazi na uwezo wa kudéveloppé kwa kufanya shughuli wakati ya mapumuziko.
- Watu wa Finland wanapenda activités extérieures kama vile kutembea musituni, kuendesha baiskeli, kuteleza kwa neje, kuvua samaki na kuogelea katika lacs au bahari.
- Watu wa Finland wanapenda kuoga ndani ya sauna. Sauna ni mahali ya kawaida ya kuoga. Sauna inaweza kupatikana katika manyumba ya watu wengi na inatumiwa mara nyingi.

- Muchezo ni muhimu katika tradition ya Finland. Watu wa Finland wanatambuliwa duniani katika muchezo mingi, kama hockey sur glace, na kushinda mashindano mingi ya dunia.
- Watu pia wanapenda kufanya muchezo mingi ili kutunza afya na maisha yao.
- Kama wewe ni athlète mudogo mwenye talanta na anayefanya bidii, c'est possible kuwa athlète professionel wa Finland.

**Ni nini inafanya Finland kuwa inchi ya technologie ya juu?**

- Mambo mingi katika jamii ya Finland iko digital na watu wengi wanatumia vitu ya technologie kama smart phone, laptop na tablet.
- Vitu tofauti ya electronique inatumiwa kila siku na shughuli mingi ya kila siku inafanywa na smart phone, kwa mufano kulipa bili, kununua vitu na kupata services publics.
- Katika professions nyingi, ni lazima kutumia technologie ili kufanya mambo ya kazini.
- Kuna kozi ya kujifunza hii mambo na ni muhimu kujifunza kutumia vitu ya digital.
- Katika familia mingi, watoto wanatumia hii vitu na technologie inaendelea kutumiwa pia shuleni na walimu.

## Video ya 2: Maisha huko Finland

**Hii ni video kwa ajili ya wakimbizi wenye wameenda kuishi huko Finland**

**Nitasafiri namuna gani kuenda Finland?**

- Ukichaguliwa kama mukimbizi inchini Finland, utapewa permis de séjour ya kudumu ya miaka inne na unaweza kupata ingine mupya baadae.
- Utapatiwa permis yako ya séjour na documents de voyage kabla ya kusafiri.
- Serikali ya Finland itapanga na kulipia safari yako ya Finland.
- Utasafiri kwenda Finland na ndege na unaweza kubadilisha ndege njiani.
- Utasaidiwa katika uwanja ya ndege.
- Unaweza kuchukua mufuko mumoja tu ya kilo 20 kwa ndege na kuongeza muzigo ya kubeba kwa mukono na isipite kilo 8.

**Nini itafanyika nikifika Finland?**

- Mipango yako ya kusafiri haitaanza mpaka wakati municipalité moja inchini Finland itakukaribisha baada ya kutayarisha nyumba yako.
- Hautaishi kwa kituo ya wakimbizi, lakini katika nyumba ya kukodisha ambayo ni nyumba yako mwenyewe.
- Huko Finland utasafiri moja kwa moja kutoka uwanja ya ndege ya Helsinki kwenda municipalité yako mupya kwa ndege, kwa basi au kwa gari.
- Baada ya kufika, utapatiwa funguo ya nyumba yako.
- Viongozi na organisations ya municipalité yako watakupatia conseils kutoka siku ya kufika, lakini lazima ukuwe na bidii ya kujifunza système mupya wewe mwenyewe.

**Nitabeba nini nikienda Finland?**

- Lazima ubebe documents yote ya kitambulisho kama passeport, makadi ya kitambulisho, permis ya kuendesha gari, certificat de naissance, kitabu ya familia nk.

- Chukua documents yote muhimu zaidi ya afya kama vile examen médical, matibabu na histoire yako ya matibabu.
- Leta pia documents muhimu zaidi ya elimu kama certificat, licence na diplôme.
- Leta certificat ya histoire yako ya kazi kama inapatikana, yenye inaonyesha umefanya kazi wapi, kazi ile ulifanya, na kwa muda gani umefanya kazi.
- Kama inawezekana, traduire hiyo documents kwa Kiingereza kabla ya kuenda Finland.
- Ni muzuri kuleta pia mapicha yako muhimu, souvenirs na vitu yako ya précieux huko Finland.

**Nitaishi namuna gani kama sijui lugha ya Finland?**

- Ni muhimu kuanza kujifunza lugha ya Finland directement, baada ya entrevue yako ya sélection ya kukuwa mukimbizi.
- Viongozi na organisations ya municipalité yako watakusaidia na kukupatia conseils ya kuandaa maisha yako ya kila siku kutoka siku ya kufika, lakini lazima ukuwe na bidii pia wewe mwenyewe.
- Attitude muzuri itakusaidia wakati wa kutulia inchini Finland.
- Viongozi wa municipalité watahakikisha umekuwa s'inscrire katika ofisi ya usajili katika municipalité hiyo ambayo utakuwa unaishi.
- Baada ya kufika, utakuwa na haki ya kuwasiliana kupitia interprète, lakini ni muhimu kuanza mara moja kusoma Finnois au Suédois, kwa sababu malugha hizi inatumiwa katika société ya Finland na huduma ya interprétation ni chache sana.
- Hutakikani kutumia watoto wako kama interprètes ingawa wanaweza kujifunza lugha mupya haraka sana.

**Kwa nini inchi na municipalité inanisaidia?**

- Unatarajiwa kusoma profession na kujisaidia pamoja na familia yako kwa kufanya kazi. Hii ni kwa wanaume na wanawake.
- Finland in inchi ya kusaidia watu na municipalité yako inakusaidia ku intégrer kabla ya kuweza kujisimamia mwenyewe.
- Communauté pia inasaidia wagonjwa, personnes rétraitees na wale ambao hawawezi kujitegemea peke yao na wanahitaji musaada zaidi.
- Système ya kusaidia watu inatoka kwa pesa ya les impôts yenye imekusanywa kutoka kwa watu wote na makampuni yote.
- Watu wote wa Finland lazima walipe les impôts, hata kama unasoma, unafanya kazi, wewe ni mugonjwa ama haufanyi kazi.
- Les impôts inatumiwa kwa hosipitali, huduma ya afya, huduma ya communauté, elimu na shule, huduma ya kutunza watoto muchana n.k.
- Kama résident du municipalité, unastahili kupata huduma ya musingi, kama vile elimu, afya na huduma ya communauté, kama watu wa Finland.
- Wakati huo huo, lazima ufate sheria na réglementations ya Finland kama watu wa Finland.

**Watu wanaweza kubadilisha municipalité?**

- Ni ngumu kuhamia municipalité ingine kabla ya kuweka pesa ya kutosha kwa ajili ya dépenses na lazima ukuwe unajua jinsi ya kufanya hivyo peke yako.

- Watu wa Finland wanaweza kuhama kutoka région moja kwenda ingine, lakini ukifika inchini Finland kama mukimbizi, inashauriwa ukae katika municipalité yako angalau miaka tano ya kwanza.
- Municipalité ya nyumba yako imejitayarisha kukukaribisha na kukupatia mahali pa kuishi pamoja na huduma na musaada muhimu.
- Ukihama haraka sana, municipalité mupya inaweza kukosa kukupatia huduma ya ku intégrer huko ambayo ni ya kibinafsi na ya muhimu sana.
- Hakuna nyumba ya bei ya chini na sio rahisi kupata nyumba mupya.
- Kama utahama, lazima utalipa dépenses wewe mwenyewe.

**Ni rahisi ku intégrer na watu wengine?**

- Kuhamia inchi mupya inaweza kuwa ngumu particulièrement wakati wa mwanzo. Inachukua muda na effort ku intégrer na watu katika communauté mupya, lakini attitude muzuri itakusaidia sana.
- Ni muhimu kuwa na passion na kuvutiwa na inchi yako mupya.
- Hata kama kutakuwa na mabadiliko mengi katika maisha yako ya kila siku, lazima ukuwe tayari kujifunza mambo mupya na ukuwe na confiance ya kujua watu wa Finland.
- Kujua lugha na réseaux sociaux itakusaidia ku intégrer na watu. Unapoendelea kujifunza Finnois au Suédois, itakuwa rahisi kujua watu wa Finland na kupata marafiki.
- Inasaidia sana kama unafata sheria na conseils ya viongozi.
- Kumbuka ni muzuri kukuwa mutu ya kuchangamuka, kwa mufano kwa kushiriki katika activités tofauti na kuanza conversations na watu wapya.

**Nitapata nyumba ya kuishi namuna gani?**

- Huko Finland utaishi katika nyumba ya kukodisha ambayo municipalité yako inapanga kwa ajili yako.
- Manyumba mingi ya municipalité imepangwa katika appartements
- Manyumba inaweza kuwa tofauti kwa dimensions na style, lakini mingi iko na chambres similaires ndani ya nyumba, ambayo ni bafu, jikoni, salon, chambre ya kulala na chambre ya watoto, ikiwa inahitajika.
- Nyumba iko na mahali moja ya kuleta joto na mwaka muzima iko joto kwa nyumba.
- Kuna électricité na maji ndani ya nyumba.

**Nyumba ya kukodisha iko na vitu ndani?**

- Kutakuwa na vitu fondamentaux tayari wakati utafika, kama vitanda au magodoro, les draps, les meubles kidogo na vyombo ya jikoni.
- Hakutakuwa na televisheni au simu kwa hiyo nyumba. Baadae unaweza kuweka pesa ya kununua vitu unahitaji kwa nyumba yako.
- Watu wa Finland wanapika chakula sana kwenye majiko ya électricité.
- Kuna réfrigérateur na wakati ingine pia kuna freezer ndani ya manyumba.
- Municipalité yako itakupatia conseils ya jinsi ya kutumia hii vitu.

**Naweza ku fumer cigarette ndani ya nyumba?**

- Kawaida hakuna ruhusa ya ku fumer cigarette ndani ya nyumba yako na majengo ingine.
- Hakuna ruhusa pia ya ku fumer cigarette ndani ya majengo na magari ya publiques.

- Hakuna ruhusa ya moto kuwaka ndani ya nyumba.

**Mutu anaweza kunywa maji ya mufereji?**

- Maji ya mufereji huko Finland ni safi sana na unaweza kunywa kutoka mufereji bila kuchemusha.
- Unaweza kupata maji ya moto na baridi kutoka kwa mufereji na shower yako.
- Lazima ulipe maji ile unatumia kwa nyumba, kwa hivyo inashauriwa usitumie maji mingi kupita kiasi.

**Nitasafiri namuna gani ndani ya municipalité?**

- Katika municipalités mingi kuna mabasi fiables ya public.
- Katika municipalités ndogo huduma fondamentaux kawaida iko karibu na manyumba ya kukodisha, kwa hivyo unaweza kupata huduma yote muhimu kwa kutembea mpaka hapo.
- Kuendesha baiskeli pia ni njia salama na ya bei ya chini ya kusafiri kama huendi mbali.
- Kutembea ni muzuri kwa afya na kawaida watu wanatembea kama kilomita 2-5 kwenda kazini au shuleni.
- Mabasi na gari moshi inatoa huduma ya safari ya kuenda mbali. Kwa kuongezea, ndege ya ndani ya inchi inapatikana, lakini bei iko juu.
- Huduma ya usafiri ya national, région na mitaa imeundwa kupatia abiria huduma fiable, salama na kamili. Kutumia transport public ni rahisi kuliko kuwa na gari ya kibinafsi.
- Teksi ni pesa mingi sana huko Finland, kwa hivyo tumia tu kama ni muhimu sana.

**Transport public ni salama kwa familia yangu?**

- Transport public ni salama kwa kila mutu.
- Wanawake wanaweza kutumia transport public peke yao.
- Watoto wanaweza kutumia transport public peke yao kwenda shule na wakati wa shughuli ya mapumziko.
- Kama mutu anasahau njia au mahali ya kushuka, madereva na abiria wengine wanaweza kusaidia.
- Kuna application ya mtandaoni ya kukupatia direction, ramani na programme ya njia ya transport public.

**Nitanunua chakula namuna gani?**

- Watu wa Finland wananunua chakula na vitu ingine kutoka kwa supermarchés.
- Siku hizi kuna maduka mingi inchini Finland ya kuuza aina tofauti ya chakula iliyoletwa inchini kutoka inchi ya Kiarabu, l'Asie na Afrika.
- Katika saison ya l'été, masoko inauza mboga frais na bizaa ingine kama champignons na matunda kutoka musituni. Masoko pia ni mahali ya watu kukutana.
- Unaweza kuchagua matunda ya musituni na champignons kutoka kwa musitu.

**Nitapata wapi pesa ya kutosha ya kununua vitu yote muhimu kwa nyumba yangu na familia?**

- Mwanzoni utapata musaada ya pesa kwa ajili ya dépenses fondamentaux ya kuishi kupitia système ya communauté. Kiasi ya musaada ni kulingana na sheria.
- Musaada yako inatosha dépenses fondamentaux na inalipwa mara moja tu kwa mwezi.

- Si muzuri kuchukua mukopo ya kulipa dépenses yako.
- Bei ya vitu huko Finland iko juu kabisa. Ni muhimu kupanga matumizi ya kila mwezi ndani ya familia.
- Ni kawaida kununua nguo, les meubles, baiskeli na vitu ya watoto katika duka ya mutumba ambapo bei iko chini sana.
- Qualité katika maduka ya mutumba inaweza kuwa ya juu sana na kuna aina mingi ya bizaa.
- Siku hizi kununua na kuuza nguo na viatu kwenye mutandao ni kitu ya kawaida.

**Finland inatumia devise gani?**

- Devise ya Finland ni euro. Ni devise ambayo inatumika na inchi mingi ya l'Union européene.
- Finland ilianza kutumia euro mwaka 2002.

**Ninaweza kutumia pesa wakati wa kununua vitu?**

- Malipo inaweza kufanywa na pesa au kadi ya benki. Hata hivyo, watu wengi sana wanatumia kadi kama njia ya malipo.
- Unahitaji akaunti ya benki ili kupata kadi ya benki.
- Ni muhimu kwa kila mukimbizi adulte kufungua akaunti yake ya benki.
- Wanaume na wanawake wako na akaunti yao tofauti ya benki.

## Video ya 3: Huduma ya watoto, elimu na droits fondamentaux kwa watoto wa Finland

**Hii ni video kwa ajili ya wakimbizi wenye wameenda kuishi huko Finland**

**Finland ni inchi muzuri kwa kulea watoto?**

- Finland inatoa services publics kwa résidents wote.
- Wanawake enceintes na watoto wa kila umri wanapata services spéciaux katika kliniki ya afya.
- Huko Finland, sheria hairuhusu watoto kusoma na kuwacha shule.
- Droits fondamentaux kwa watoto ni pamoja na droits ya afya, elimu, maisha ya familia, muchezo, maisha bora na kulindwa kutokana na mateso na kuumizwa.

**Méthode ya kulea watoto ni tofauti huko Finland?**

- Wazazi wote duniani wanataka maisha bora kwa watoto wao. Lakini méthodes ingine ya kulea watoto inaweza kubadilika ukifika Finland.
- Mahitaji ya watoto lazima ikuwe addressées na ni lazima kuishi katika mazingira salama na kuwa na relation muzuri, ya karibu.
- Wasichana na wavulana lazima wakuwe traités de manière égale, na kufurahia haki sawa katika maisha yao yote.
- Lazima utunze maisha ya watoto wako kabisa hadi wakue adultes.
- Katika sheria ya Finland, watoto wanakuwa adultes wanapofika miaka 18.
- Kama uko na problème ya kulea watoto au relation ya familia, unaweza kuomba musaada kutoka kwa service ya garderie, shule au service ya conseils ya familia ya municipalité.

**Ninaweza kumuchapa mutoto wangu?**

- Huko Finland kuchapa mutoto ni makosa.
- Huwezi kuazibu watoto kwa kupiga kofi au kuvuruta nywele. Kunyanyasa watoto kwa njia yoyote ni makosa.
- Kuna méthodes tofauti ya kulea na kuazibu mutoto ambayo ni effectif.
- Hii méthodes tofauti inaweza kuwa discutés na wafanyikazi wa communauté na wa afya, service ya garderie na shule.

**Nani anachunga watoto muchana kama wazazi wanasoma au wameenda kazini?**

- Municipalités yote inatengeneza elimu ya watoto wadogo katika garderie kwa watoto chini ya miaka saba na shule ya mapema kwa watoto wa miaka sita.
- Wazazi wote wanaweza kufanya kazi au kusoma wakati watoto wako katika garderie.
- Huko garderie hao wanacheza na kujifunza compétences tofauti muhimu wakati wa kuanza shule ya musingi. Walimu wa garderie wamesoma kabisa.
- Watoto wa watu wa inchi ingine wanajifunza Finnois au Suédois haraka sana wakati wanakutana na watoto wengine huko garderie.
- Watoto wa garderie wanapatiwa chakula yote muhimu.
- Watoto wanaweza kuanza garderie hata kabla ya mwaka mumoja ikiwa wazazi wanafanya kazi au wanasoma.
- Ni muzuri mutoto wako kuanza garderie kama amechelewa sana, akiwa na miaka tatu ili ajifunze lugha ya Finnois au Suédois.

**Elimu ya watoto wadogo ni ya bure?**

- Kuna pesa ya kulipa kutegemea mapato ya familia yako na watoto wako ni wangapi.
- Kawaida watu wanalipa elimu ya watoto wadogo kama wanafanya kazi na wanapata mushahara ya kutosha.
- Watu wa mapato kidogo hawalipi kitu, lakini watoto wao wanapata services sawa na wengine.

**Mutoto anaenda shule na miaka ngapi huko Finland?**

- Watoto wanaanza darasa ya kwanza ya elimu wakiwa miaka saba.
- Watoto wote inchini Finland lazima waende shule.
- Elimu ya shuleni kawaida inadumu miaka tisa kwa watoto wa umri wa miaka 7-16.
- Watoto wenye hawezi kuongea Finnois au Suédois wanapokea musaada zaidi katika kujifunza hiyo lugha.

**Siku ya shule katika shule ya musingi iko namuna gani?**

- Siku ya shule inaweza kuanza wakati tofauti kwa siku tofauti. Kwa kawaida, siku ya shule inaanza saa mbili au saa tatu asubuhi kutoka Jumatatu hadi Ijumaa.
- Katika siku ya shule kuna masomo tofauti kama lugha, hesabu, biologie, histoire na michezo.
- Watoto wanacheza inje wakati wa kupumuzika.
- Watoto wote wanakula chakula ya muchana ile joto huko shuleni.
- Walimu wanaweza kupatia watoto devoirs kila siku.
- Siku ya shule inaisha kawaida kati ya saa sita na saa nane muchana.

**Kazi ya wazazi ni nini kwa masomo ya watoto?**

- Kama muzazi lazima kuangalia kwamba watoto wako wanaenda shule kwa masomo yote kila siku.
- Lazima ujulishe shule mara moja kama watoto wako hawataenda shule kwa sababu ya ugonjwa au sababu ingine.
- Lazima uangalie kuwa watoto wako wanamaliza devoirs ambayo walipewa na walimu.
- Shule na wazazi wa Finland wana communiquer mara kwa mara kuhusu progrès ya wanafunzi.

**Watoto wanaweza kufanya nini wakati wa kupumuzika?**

- Ni muhimu kwa watoto kufanya activités wakati ya kupumuzika kwa sababu wanaweza kujifunza lugha na kupata marafiki wa Finland.
- Kuna mambo tofauti ya kuchagua kufanya wakati wa kupumuzika kwa ajili ya watoto huko Finland.
- Iko nafasi ya kucheza muchezo, dansi, muziki, sanaa ya kuchora au théatre, kozi za kupika, na ingine mingi.
- Shule mingi, centres ya vijana, organisations na bibliothèque publique inapanga activités tofauti ya wakati ba kupumuzika kwa ajili ya watoto.

**Hii activités ni ya bure?**

- Activités ingine kama vilabu ya muchezo, lazima kulipa pesa, lakini pia kuna activités mingi ya bure kabisa.
- Familia inaweza kufurahia shughuli mingi ya wakati wa kupumuzika pamoja bila dépenses yoyote kama kutembelea uwanja ya muchezo, bibliothèque publique, na sherehe ya kitamaduni na muchezo.
- Ni muhimu familia ku passer les temps pamoja na kupeleka watoto wao kucheza.

## Video ya 4: Opportunités ya elimu na maisha significatifs kwa vijana

**Hii ni video kwa ajili ya wakimbizi wenye wameenda kuishi huko Finland**

**Système ya elimu iko namuna gani huko Finland?**

- Système ya elimu ya Finland inajulikana kwa qualité ya juu sana. Inatoa opportunités sawa ya elimu kwa kila mutu, haijalishi mtu ako na miaka ngapi.
- Elimu ya Finland iko na shule ya musingi (darasa ya 1-6) na shule ya secondaire (darasa ya 7-9), elimu ya secondaire supérieure na université. Masomo yote ni ya bure.
- Shule ni kwa watu wa chini ya miaka 18.
- Municipalité yako itapanga mahali ya kusoma katika shule ya endroit yako na utapatiwa musaada ya kujifunza Finnois au Suédois.
- Mwalimu wako ata analyser ni darasa gani muzuri zaidi kwako, kulingana masomo yako ya zamani na umri yako.
- Ukifika Finland na miaka 17 au zaidi, unaweza kusoma elimu yote ya shule ya secondaire katika shule ya elimu ya secondaire supérieure ya adulte.
- Huko Finland masomo imetengenezwa kwa ajili ya wanafunzi tofauti ili kila mwanafunzi aweze kumaliza masomo yake na kuingia université au kufanya kazi.

**Ninaweza kusoma kwa Finnois au Suédois?**

- Baada ya darasa ya préparation ya mwaka mumoja au musaada inayofanana na hiyo ya kupata mambo muhimu ya lugha, utapokea musaada kwa Finnois au Suédois wakati wote wa masomo.
- Kiingereza inafundishwa shuleni kama lugha ya pili na kuna lugha mingi ingine ambayo unaweza kusoma, lakini shule itachagua.

**Ninaweza kufanya kazi baada ya shule ya secondaire?**

- Sio kawaida au rahisi kuanza kufanya kazi baada ya shule ya secondaire.
- Kuna kazi chache tu kwa watu bila elimu. Kwa hivyo, unashauriwa kusoma zaidi huko Finland.
- Baada ya shule, unaweza kuingia elimu ya secondaire supérieure kwa masomo zaidi, au unaweza kusoma katika école professionel. Masomo yote mbili itachukua mwaka tatu.
- Baada ya kumaliza école professionel, unaweza kuanza kutafuta kazi au mahali ya kufanya apprentissage.
- Tayari wakati ya masomo, kuna muda mingi ya kufanya apprentissage, na hapo unaanza kuzoea kazi.
- Kuna nafasi mingi ya wewe kufanya kazi ya muda mufupi wakati wa mapumuziko yako na likizo ya shule ili kupata argent de poche.
- Kutoka mwaka 15 unaweza kusigner contrat ya kazi wewe mwenyewe. Kabla ya hapo contrat lazima ikuwe signer na muzazi.

**Ninaweza kufanya nini wakati wa kupumuzika?**

- Municipalité na organisations tofauti inatoa nafasi mingi ya activités ya wakati wa kupumuzika kwa vijana na mingi ni ya bure.
- Unaweza kuchagua mwenyewe aina ya activités ya wakati ya kupumuzika kutoka aina tofauti ya muchezo hadi muziki, dansi, sanaa, activités ya inje na kazi ya volontaire.
- Kuna espaces wazi na uwanja kwa muchezo ya nje ambayo inaweza kutumiwa na mutu yoyote.
- Bibliothèques publiques mingi iko na maeneo maalumu kwa vijana kupumuzika na kucheza muchezo na kukutana na vijana wengine baada ya masaa ya shule na jioni.
- Unaweza kuomba vitabu kwa lugha tofauti bila dépenses yoyote kutoka kwa bibliothèque publique yako.

**Relation ya mapenzi na mariage iko namuna gani huko Finland?**

- Vijana na adultes wanajuana kupitia période de séduction. Hii inapatia watu wanaopendana nafasi ya kujuana.
- Si lazima séduction ilete relation ya mariage.
- Huko Finland, ni kawaida kuwa na relation ya mapenzi kabla ya mariage.
- Umri ya chini wa inchi kwa ajili ya mariage ni 18 kwa sexes yote mbili.
- Wanawake na wanaume wako na haki ya kuchagua ni nani wanataka kuséduire na marier; wanaamua wenyewe wanataka kuishi na nani.
- Hakuna mutu anaweza kulazimishwa kuséduire au marier.
- Unaweza kuazibiwa na sheria ukilazimisha mutu mariage, awe ni mwanaume au mwanamuke.
- Huko Finland unaweza kuwa na bwana au bibi mumoja tu wakati mumoja.

- Huko Finland, mutu yoyote anaweza kupata divorce na haitaji kutegemea époux wa zamani kwa musaada ya pesa.

**Relation sexuelle inaruhusiwa kabla ya mariage?**

- Wasichana na wavulana wanafanya urafiki na kushirikiana kwa uhuru hata na sexe tofauti. Hata hivyo, séduction haimaanishi kwamba vijana wakuwe na relation sexuelle.
- Ni legal na inakubalika kwa jeune couples kuishi pamoja na kuwa na relation sexuelle kabla na hata bila mariage.
- Umri ya kukubali mambo ya sexuelle huko Finland ni miaka 16.
- Hii njo umri ya chini kabisa ya mutu kuonekana kutosha kisheria kuweza kukubali kushiriki katika mambo ya sexuelle.
- Kila mutu huko Finland ako na droit ya kisheria ya kumukataa mutu mwingine kumushika kwa mwili. Hakuna mutu, hata époux, ambaye anaweza kulazimishwa kufanya rapports sexuels bila kukubali.

**Ninaweza kuanza familia na mutu wa Finland?**

- Uko na huru kuanzisha familia na mutu yoyote unayesikilizana nayeye na kukubaliana kuhusu hiyo relation.
- Watu wa inchi tofauti kufanya mariage na kuanzisha familia inaongezeka huko Finland.
- Watu wa Finland wanachagua fiancés wao wenyewe na hakuna ruhusa inahitajika kutoka kwa wazazi au familia.
- Kabla ya kuanzisha familia, ni muhimu kwamba nyinyi wawili mujadiliane kabisa kuhusu valeurs, matamanio ya baadae, intêret ya kupata watoto na maneno ingine muhimu ambao ita affecter maisha ya mariage.
- Les époux wanaweza kuuliza maoni ya familia yao, lakini familia au wazazi lazima waheshimu droits ya mutu binafsi ya kuchagua mupenzi wake.

**Ninaweza kuteswa au kukuwa discriminé kwa sababu ya inchi yangu na mutazamo tofauti?**

- Kuteswa na kukuwa discriminé ni makosa inchini Finland na kila mutu ni sawa katika sheria ya Finland.
- Katika mashule na services yote ya public, kuteswa na kukuwa discriminé ni makosa kabisa.
- Ikiwa wewe mwenyewe uko tayari kukutana na watu wapya na kujaribu kutumia Finnois au Suédois, itakuwa rahisi ku intégrer na watu wa Finland.
- Shule, burudani na sherehe ya vijana ni nafasi muzuri ya kupata marafiki wapya.

## Video ya 5: Elimu na maisha ya kufanya kazi kwa adultes

**Hii ni video kwa ajili ya wakimbizi wenye wameenda kuishi huko Finland**

**Hatua ya kwanza baada ya kufika Finland ni gani?**

- Kama wewe ni adulte mwenye afya muzuri na uko na miaka 17-64, lazima uregistrer katika services publics de l’emploi kama mutu asiye na kazi ambaye anatafuta kazi.
- Viongozi na washauri watakusaidia kuelewa hii mambo yote.

- Compétence yako ya lugha na kazi yako ya zamani itaangaliwa, na utapata mupango ya kibinafsi ya ku intégrer na watu.
- Ofisi ya kazi itakuandikisha katika kozi ya ku intégrer na watu ya kukupatia compétence ya lugha, kuelewa société ya Finland na maisha ya kufanya kazi. Pia utafanya apprentissage.

**Itakuwaje kama siwezi kufanya kazi?**

- Kama hutaonekana kuwa na uwezo wa kufanya kazi, kama vile walemavu, watu zaidi ya miaka 64, mama ya kuchunga watoto wadogo nyumbani nk. hauitaji kujiandikisha katika services publics de l'emploi.
- Kama wewe ni wa hii kikundi, unatayarisha mupango yako ya ku intégrer na watu pamoja na ofisi ya kijamii ya municipalité yako.
- Mupango wa ku intégrer na watu itakuongoza kupata kozi muzuri ya lugha na activités ingine yenye maana kama vile vikundi tofauti ya kushughulika.
- Hata kama huwezi kufanya kazi, ni muhimu sana kusoma lugha hiyo mupya na kufahamu société ya Finland.
- Unatarajiwa pia kutunza afya na maisha yako.

**Itakuwaje kama sijui kusoma au kuandika?**

- Kuna kozi spécial ya ku intégrer na watu kwa wale ambao hawajui kusoma na kuandika. Hakuna haja ya kusoma au kuandika kabla ya kufika Finland au unaweza kusoma au kuandika kwa lugha yako peke yake.
- Kozi ya watu ambao hawajui kusoma na kuandika inaenda polepole ili kila mutu aweze kujifunza compétences fondamentaux wa kusoma.
- Baadae unaweza kujiunga na kozi ya juu zaidi ya ku intégrer na watu.

**Adultes wa inchi ingine wenye hawajamaliza shule yao wanaweza kuenda shule?**

- Kama hujamaliza shule katika inchi yako na bado wewe ni mudogo, unaweza kujiandikisha katika shule ya elimu ya secondaire supérieure kwa adultes.
- Huduma za kazi kwa public itatoa miongozo zaidi na kukusaidia kujiandikisha katika kozi ambayo inafaa zaidi kwako.

**Naweza kuanza kufanya kazi mara moja baada ya kufika inchini Finland?**

- Kama mukimbizi unapatiwa permis de travail na droit ya kufanya kazi unapofika Finland. Droit yako ya kufanya kazi imeandikwa katika kadi yako ya permis de séjour.
- Unaweza kufanya kazi ya muda mufupi pamoja na masomo yako ingine.
- Hata hivyo, huko Finland, ni ngumu kupata kazi bila certificat rasmi iliyopatikana kutoka kwa masomo na compétences ingine muhimu.
- Ni muhimu sana kujifunza compétences fondamentaux katika lugha ya Finnois au Suédois. Ni muhimu kuanza kujifunza maneno ya musingi hata kabla ya kufika Finland.
- Unaweza kupata kazi kupitia services ya kazi ya public na ya kibinafsi au kwa kuwasiliana na waajiri moja kwa moja.
- Kuna kazi ya muda mufupi na ya muda yote. Masaa ya kawaida ya kufanya kazi ni masaa nane kwa siku.

**Ni aina gani ya kazi inapatikana katika marché de l'emploi ya Finland?**

- Sécurité sociale, huduma ya afya, elimu ya watoto wadogo na kusafisha ni kazi inayohitajika sana kwa wafanyikazi katika sehemu tofauti ya Finland.
- Pia kuna nafasi muzuri ya kazi katika ujenzi, kazi ya mutambo, upishi, misitu na usafirishaji.
- Kujua Finnois au Suédois ni muhimu katika kusoma shuleni na maisha ya kufanya kazi.

**Ninaweza kuanzisha biashara yangu mwenyewe huko Finland?**

- Kuwa mutu wa biashara ni njia moja ya kupata mapato yako mwenyewe inchini Finland.
- Kuna watu wa biashara wa inchi ingine ambao wamefanikiwa, kwa mufano katika upishi, kuuza maduka, kuuza manyumba, ujenzi, usafirishaji na huduma ya kijamii.
- Kabla ya kuanzisha biashara, lazima ujuwe sheria ya Finland, système ya les impôts, mazingira ya biashara na mahitaji ya kuanza biashara.
- Kujua lugha ya Finnois ni muhimu katika biashara.
- Unaweza kupokea musaada ya pesa kwa wakati ya kwanza ya kuanzisha biashara ikiwa mupango yako ya biashara imekubaliwa na service ya kazi.

**Ninaweza kusoma profession huko Finland namuna gani?**

- Kama tayari uko na digrii, unaweza kugundua jinsi ya ku transfert kwa digrii kama yako huko Finland. Mara mingi utaulizwa kufanya masomo ya kuogezea huko Finland.
- Ecoles mingi ya profession huko Finland inatoa aina mingi ya masomo ya ufundi na mupango ya mafunzo, na kupatia watu certificat kwa aina tofauti ya kazi.
- Masomo inachukua kawaida miaka mbili hadi tatu.
- Ecoles ya profession inatoa masomo ya kuongezea ya lugha na musaada kwa watu ambao lugha yao ya mama sio Finnois au Suédois.
- Kuna aina tofauti ya écoles ingine ya elimu ya juu, kama vyuo vikuu ya sayansi na universités.
- Huko Finland, elimu yote ya juu ni ya bure.

**Wanawake wanaweza kufanya kazi ya namuna gani huko Finland?**

- Huko Finland ni kawaida kabisa kwa wanaume na wanawake kufanya aina yoyote ya kazi.
- Kwa mufano, wanaume wanaweza kuwa walimu ya garderie au wauguzi na wanawake wengi wanafanya kazi ya mukono au madereva ya mabasi.
- Wanawake wote wanatarajiwa kusoma profession na kuingia katika maisha ya kufanya kazi.
- Système ya garderie inasaidia wanawake kupata kazi permanent hata kama wako na watoto wadogo.

**Kama mama ya familia pia anafanya kazi, ni nani anatunza nyumba?**

- Huko Finland majukumu ya wazazi na ya nyumbani imegawanywa également kati ya wanaume na wanawake.
- Wazazi wawili wanafanya kazi ya kupika, kusafisha, kununua vitu kwa duka na kutunza watoto.
- Wakati kila mutu ya familia anaenda shule na kufanya kazi, majukumu ya nyumbani inahitaji kugawanywa également kati ya watu wote wa familia.
- Katika mashule ya secondaire ya Finland, wavulana na wasichana wanafundishwa jinsi ya kupika chakula, kusafisha nyumba na kutunza nyumba yao muzuri.

## Video ya 6: Huduma ya sécurité sociale na services ya afya huko Finland

**Hii ni video kwa ajili ya wakimbizi wenye wameenda kuishi huko Finland**

**Sécurité sociale imetengenezwa namuna gani huko Finland?**

- Kama uko na afya muzuri na uko chini ya miaka 65, unatarajiwa kufanya kazi kwa wakati wote na kujisaidia wewe na familia yako na mapato ya kutoka kazini.
- Kila mutu analipa les impôts kutoka kwa mapato yake ili kulipia gharama ya services ya publics.
- Les impôts inatolewa pia kutoka marupurupu ya kijamii.
- Finland ni jamii ya kujali watu ambayo inamaanisha kwamba ikiwa mutu hafanyi kazi, ni mugonjwa, mulemavu au muzee, serikali inapatia yeye mahitaji yake fondamentaux.
- Services yote ya sécurité sociale wanatoka kwa les impôts.

**Ninaweza kupata sécurité sociale huko Finland?**

- Kama mutu ya kukaa kwa municipalité uko na droit ya sécurité sociale inchini Finland kama wewe unahitaji. Hii ni pamoja na services tofauti ya kijamii na faida ya kijamii katika hali tofauti ya maisha.
- Taasisi ya Bima ya Jamii ya Finland, Kela, inatoa services kwa watu wote wanaoishi kwa municipalité katika mambo ya sécurité sociale.

**Système ya sécurité sociale inatoa huduma kwa wazee na walemavu?**

- Municipalité iko na responsabilité ya musingi ya kutunza wazee na walemavu.
- Municipalité inaweza kutoa mahitaji maalumu ya nyumba kama vile kuingia kama uko na kiti ya magurudumu.
- Services ya kibinafsi ya wazee na walemavu inapatikana katika municipalités na katika hospitali kuu.
- Wazazi wa mutoto mulemavu sana wanaweza kupata musaada ya pesa ya kusaidia dépenses kwa ajili ya mutoto.
- Watoto walemavu wanaenda shuleni na kupata musaada spécial kutoka kwa walimu.

**Faida ya familia ya aina inatolewa kwa wazazi inchini Finland?**

- Uko na droit ya kutumia service ya kliniki ya uzazi wakati ya kukuwa enceinte na baada ya kuzaa.
- Kliniki ya uzazi inaangalia afya yako na afya ya mutoto.
- Wanawake wengi wanazala katika hospitali ya hali ya juu.
- Baada ya kuzala mutoto, unaweza kumutunza mutoto nyumbani.
- Wakati huu, musaada ya pesa inapatikana kwa muzazi anayelea mutoto, ambaye anaweza kuwa mama au baba.
- Huko Finland, imekua kitu ya kawaida kwa baba kukaa nyumbani na kuwatunza watoto wakati mama anafanya kazi.

**Niko na droit ya kutumia services ya afya huko Finland?**

- Unapatiwa service ya afya ya municipalité également na watu wa Finland.

- Upimaji wa afya imeandaliwa kwa wakimbizi wote na familia yao wanapofika kwa municipalité yao mupya. Hii itaruhusu wafanyikazi wa afya kuamua kama mutu anahitaji services yoyote ya afya.
- Ni muhimu kufata prescription yako na information ya matibabu wakati ya kusafiri.
- Huko Finland, professionnels wote wa huduma ya afya na interprètes wa kisheria lazima wasitoe siri ya watu.

**Nitapata services ya afya ya namuna gani?**

- Kama résident ya municipalité utawekwa ndani ya système ya services ya afya ya public.
- Services ya afya ya public banatoa services fondamentaux ya matibabu, lakini kuna tofauti kazaa ya jinsi hii services inapangwa katika municipalités tofauti.
- Services ya afya ya watoto inaanzia wakati wa kuzala hadi wakati wa kumaliza shule.
- Maitaji yako kwa services yoyote ya afya na huduma spécial ya afya itachunguzwa na kupelekwa kwa huduma inayofaa ikiwa ni lazima.
- Kama umepata mateso au vurugu, unaweza kupata musaada ya psychologie na aina ingine za usaidizi. Hii service inapatikana kwa watu wa kila umri.

**Itakuwaje nikikuwa mugonjwa wakati wa kufanya kazi?**

- Kila mutu anayeishi inchini Finland ako na assurance maladie ya kitaifa, kutoka kwa muchango ya watu wote walio na assurance emploi.
- Ukikuwa mugonjwa au kupata ajali, uko na droit ya kukaa nyumbani, lakini lazima umupatie employeur wako barua ya daktari.

**Watu wanapata services ya afya kuhusu mambo yao ya sexe?**

- Vituo ya afya na kliniki yao ya uzazi inatoa conseils ya bure kwa mambo ya sexe na uzazi.
- Magonjwa ya zinaa inatibiwa katika vituo ya afya au kliniki maalumu. Vituo ya afya inatoa vipimo vya HIV na dawa ya wagonjwa wa HIV inchini Finland ni bure.

**Services ya afya ya public inashughulikia services ya meno?**

- Kama résident ya municipalité uko na droit ya kutumia services ya meno ya public.
- Wakimbizi wote watapitia ukaguzi ya meno na watapata conseils ya jinsi ya kutunza meno yao kwa mambo ya chakula na usafi.
- Kama daktari yako ya meno atagundua unaitaji utunzaji ya meno au chirurgie, utapata rendez-vous ya hii service.

### Ninaweza kutumia prescription yangu ya zamani kutoka inchi yangu nikifika Finland?

- Huko Finland, daktari anaandika dawa ya ugonjwa. Utapata prescription ambayo lazima upeleke kwa duka ya dawa ili kununua dawa yako.
- Kama uko na ugonjwa wa muda murefu, chukua prescription yako ya zamani kwa rendez-vous ya daktari huko Finland.

Unakaribishwa sana kuanza maisha yako mupya inchini Finland! TERVETULOA!